

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA



TANGAZO LA KUITWA KAZINI

Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI) inapenda kuwataarifu waombaji kazi wa nafasi mbalimbali za kada za afya waliowasilisha maombi kuanzia tarehe **22/07/2019** hadi tarehe **05/08/2019** kuwa mchakato wa kuwapangia vituo vya kazi umekamilika.

Waombaji wote wanatakiwa kuzingatia maelekezo yafuatayo:-

- i) Waombaji wote wanatakiwa kuripoti katika vituo vya kazi walivyopangiwa katika muda wa siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya tangazo hili. Aidha, waombaji watakaoshindwa kuripoti kwenye vituo vya kazi ndani ya siku kumi na nne (14) nafasi zao zitajazwa na waombaji wengine haraka iwezekanavyo.
- ii) Waombaji wote wanatakiwa kuwasilisha vyeti halisi (**Original Certificates**) vya Kidato cha Nne, Sita, Chuo Kikuu, NACTE na vyeti halisi vya usajili wa mabaraza ya kitaalam kwa ajili ya kuhakikiwa na mwajiri kabla ya kupewa barua ya ajira.
- iii) Waombaji wote watakaoripoti na **Transcript tu** au bila ya kuwa na vyeti halisi (**Original Certificates**) vya Kidato cha Nne, Kidato Sita, Chuo Kikuu, NACTE na vyeti halisi vya usajili wa mabaraza ya kitaalam hawatapokelewa.
- iv) Waombaji waliopata nafasi za ajira wanajulishwa kuwa hakutakuwa na nafasi ya kubadilisha vituo vya kazi walivyopangiwa. Waombaji

watakaoshindwa kuripoti katika vituo walivyopangiwa kwa muda uliopangwa, nafasi zao zitajazwa na waombaji wengine wa kada husika.

Waombaji wote ambao majina yao hayakuonekana katika tangazo hili, watambue kuwa hawakupata nafasi hivyo wasisite kuomba kwa mara nyingine nafasi za kazi zitakapotangazwa.

Wakurugenzi wote wa Mamlaka za Serikali za Mitaa wanaelekezwa kuwapokea, kuhakiki vyeti na kuwafanyia mafunzo elekezi (Induction Course) kabla ya kuwapangia vituo vya kazi.

Orodha ya majina ya waombaji waliopangiwa vituo vya kazi inapatikana kupitia tovuti ya OR-TAMISEMI www.tamisemi.go.tz.

Limetolewa na:

Katibu Mkuu,

Ofisi ya Rais - TAMISEMI,

Mji wa Serikali - Mtumba,

S.L.P. 1923,

DODOMA.

18 Septemba, 2019